# MWANAMKE NA JINSIA

SAUTI YA WANAWAKE TANZANIA

Toleo Na. 6, 2016



TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA

# TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA

# SAUTI YA WANAWAKE TANZANIA NA 6 MWANAMKE NA JINSIA

**TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA**
**S.L.P 20679**
**Dar es Salaam,**

© *Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima 2007*
*Chapisho la Kwanza 2007*
*Chapisho la Pili 2016*

**ISSN 1821- 598X**

**Haki zote zimehifadhiwa. Si ruhusa kwa mtu yoyote kuchapisha au kunakili sehemu ya kitabu hiki bila ruhusa ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.**

# Dibaji

Jarida hili ni la sita katika mfululizo wa majarida ya "Sauti ya Wanawake Tanzania". Jarida linazungumzia changamoto za kijinsia katika jamii ya Tanzania; jinsi wanawake wanavyoathirika na wanavyoweza kuzikabili.

Madhumuni mahsusi ya mpango wa majarida haya ni kuwawezesha wanawake kujadili matatizo yanayokwamisha maendeleo yao kwa ujumla, kijamii, kiuchumi, kiutamaduni, kisiasa na kutafuta mbinu za kuyatatua kwa ushirikiano.

Jarida hili limeandikwa baada ya majadiliano na makundi mbalimbali, kuhusu changamoto za kijinsia katika jamii ya Tanzania na jinsi ya kuzitatua. Waliohusika ni viongozi wa serikali za mitaa, wanawake wajane, wajumbe wa baraza la mahakama, wazee maarufu, wanawake na asasi zisizo za serikari, katika mikoa ya Mwanza, Kilimanjaro, Njombe, Mbeya na Dar es Salaam.

Lugha iliyotumika kuandika jarida hili ni rahisi na fasaha ili walengwa na jamii nzima waweze kulisoma na kuelewa ujumbe uliomo.
Ni matumaini yetu kwamba jarida hili litahamasisha wanawake wote na jamii kwa ujumla kutafakari masuala mbalimbali ya kijinsia yaliyopo katika jamii zetu na kuyatafutia ufumbuzi.

Dkt. F. M. S. Mafumiko
**Mkurugenzi**
**TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA**

# Shukrani

Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, anatoa shukrani za dhati kwa wale ambao kwa njia moja au nyingine wamechangia katika kukamilisha jarida hili.

Kazi hii isingekamilika kama sio jitihada za pekee za wajumbe kutoka Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, wajumbe hao ni:

**Waliofanya Utafiti:**
Mugabe Mtani,
Dkt. Kapinga Bernadetha,
Leonia Kassamia,
Rehema Maganga,
Placid Balige,
Marietha Mrutu,

**Walioshiriki Katika Warsha ya Uandishi wa jarida hili ni:**
Herry Lugala,
Habibu Muyula,
Frank Mbele,
Justine Mbwambo,
Dkt. Kassimu Nihuka,

**Viongozi Warsha:**
Mugabe Mtani,
Dkt. Kapinga Bernadetha,

**Mhariri:**

Eric Samba,

**Mchapaji:**

Zena Rajabu Kazala,

**Msaidizi:**

Said Mapande.

**Msanifu:**

Rehema Maganga

**Dkt. Fidelice M. S. Mafumiko**
**MKURUGENZI**

# Yaliyomo

**Dibaji** .......... iii

**Shukrani** .......... iv

**Utangulizi** .......... vii

**Sura ya Kwanza** .......... 1

Maana ya Jinsia .......... 1

**Sura ya Pili** .......... 3

Nafasi na wajibu wa mwanamke katika kupambana na unyanyasaji wa kijinsia .......... 3

**Sura ya Tatu** .......... 5

Athari za ukiukwaji wa Usawa wa Kijinsia .......... 5

Athari za ukiukwaji wa usawa wa kijinsia .......... 5

**Sura ya Nne** .......... 8

Mifumo, Mila na Desturi zinazochangia Unyanyasaji wa Kijinsia .......... 8

**Sura ya Tano** .......... 13

Jitihada Zinazofanywa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima katika Kuleta Usawa wa Kijinsia .......... 13

**Sura ya Sita** .......... 16

Jitihada za serikali na mashirika binafsi kupambana na unyanyasaji wa kijinsia .......... 16

Kuwapa wanawake uwezo wa kisheria .......... 16

# Utangulizi

Uelewa wa wanawake juu ya masuala ya kijinsia ni muhimu kwa maendeleo ya jamii. Juhudi mbalimbali zimefanyika nchini kwa lengo la kuwawezesha wanawake kutambua haki zao na kuishi maisha bora. Ingawa bado wanawake wana changamoto zinazowakabili katika maisha yao.

Hivyo basi lengo la utafiti huu ni kuibua masuala mbalimbali ya kijinsia katika jamii na kuyatafutia ufumbuzi. Matokeo ya utafiti huu yametumika kama msingi wa uandishi wa jarida hili. Pia taarifa hizi zimewawezesha waandishi kuandika habari zinazoonesha uhalisia wa changamoto zinazowakabili wanawake na kupendekeza njia mbalimbali za kukabiliana nazo.

Sampuli lengwa na `sampulishaji holela zilitumika katika kupata wilaya sita za Tanzania bara ambazo ni Nyamagana, Tarime, Iringa vijijini, Siha na Mbalali. Sampuli lengwa na usampulishaji holela pia zilitumika kupata walengwa 126 ambao ni: wanawake wajane, wanawake walio katika ndoa za mitala, wajumbe wa baraza la mahakama/mila na desturi na wazee maarufu au viongozi wa vijiji/ kata/vitongoji.

Njia zilizotumika katika ukusanyaji wa taarifa ni majadiliano ya vikundi na hojaji. Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa wanawake wanagandamizwa na mfume dume ambao unajumuisha: Ukeketaji, ndoa za umri mdogo, kutokuwa na haki ya kumiliki mali, kurithi wajane na utoaji wa adhabu kama vile vipigo.

Pia matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa wanawake wana majukumu mengi ya kutekeleza ambayo yana mchango

mkubwa katika familia kama vile: kulea watoto, kupika chakula, kuchota maji, kulima mashamba, kuvuna na kutafuta kuni. Vilevile matokeo ya utafiti yamedhihirisha kuwa baadhi ya wilaya kama vile Iringa Vijijini na Nyamagana zimeanza kuunga mkono juhudi za serikari kwa kujiwekea mikakati mbalimbali ya kuwasaidia wanawake kukabiliana na mifumo gandamizi. Hali kadhalika utafiti umeonesha kuwa katika wilaya za Mbalali, Nyamagana na Iringa Vijijini wanawake wameonesha kutambua haki zao ingawa hawajabadilisha mitazamo yao katika jamii kama vile umiliki wa mali, urithi na ndoa za utotoni.

# Sura ya Kwanza

## Maana ya Jinsia

Dhana ya jinsia ni mahusiano yaliyojengwa na yanayoendelea kujengwa na jamii pamoja na kutambua tofauti za kimaumbile, mgawanyo wa majukumu ya kazi, mgawanyo wa mapato na rasilimali nyingine, fursa sawa za kushiriki katika siasa na utawala, mila na desturi mbalimbali n.k, kati ya wanaume na wanawake.

Masuala ya jinsia yanalenga zaidi mahusiano yaliyopo kati ya mwanamke na mwanaume katika mgawanyo wa kazi, mali na mahitaji muhimu.

Hivyo basi, jinsia ni malezi na makuzi yaliyojengeka katika jamii ambayo hutofautisha kati ya jamii na jamii. Jinsia ni dhana muhimu ya kutafakari kuhusiana na ujenzi na uendelezaji wa mahusiano yaliyo sawa katika jamii.

Mara nyingi jinsia katika jamii na familia kwa jumla imekuwa ikihusisha mwanamke peke yake, uelewa ambao hauendani na maana halisi ya tafsiri ya jinsia. Hivyo basi familia na jamii zinapaswa kubadilisha mtazamo huo ili kuleta ustawi wa jamii.

Neno jinsia linatambulika na kutumika karibu na makundi yote ya jamii. Hata hivyo utafiti umeonesha kuwa karibu nchi zote wanawake ndio wanaathirika kutokana na uelewa finyu wa masuala ya kijinsia. Hii huchangiwa na baadhi ya mila na desturi na hali duni ya kiuchumi.

Aidha, inaonesha kuwa wanawake na wasichana wengi wanafikiri kuwa shughuli zote za nyumbani kama vile kupika, kulima, kulea *watoto na kutunza familia ni jukumu la mwanamke. Hali hii* huchangia kwa kiasi kikubwa wanawake na wasichana kukosa nafasi ya kwenda shule hivyo kubaki na hali duni. Elimu ya jinsia kwa wazazi, na jamii nzima ni muhimu; na pia wanawake na wanaume wanapaswa kupewa nafasi sawa katika elimu.

# Sura ya Pili

## Nafasi na wajibu wa mwanamke katika kupambana na unyanyasaji wa kijinsia

Mwanamke anayo nafasi na wajibu mkubwa katika familia na jamii kwa ujumla katika kupambana na unyanyasaji wa kijinsia. Katika sura hii nafasi na wajibu wa mwanamke kama mzazi, mlezi na mshauri inajadiliwa.

## Mwanamke kama Mzazi

Mwanamke anao wajibu mkubwa kwa familia na jamii kwa vile yeye ndiye anayebeba na kulea mimba hadi mtoto anapozaliwa. Hivyo hana budi kujitahidi kupambana na unyanyasaji wa kijinsia ambao unaweza kumwathiri yeye pamoja na familia yake. Asipopambana matokeo yake atakosa haki yake na haki ya familia na hivyo kuwa masikini.



*Kielelezo: mama akiwa na watoto wake*

## Mwanamke kama Mshauri

Mwanamke ni mshauri wa familia majirani hata marafiki. Hivyo hii ni nafasi nyingine ambayo wanawake wanaweza kuitumia kupambana na unyanyasaji wa kijinsia kwa kutumia vipaji vyao vya ushauri. Wanawake hawana budi kuzishauri familia na jamii nzima namna ya kupambana na unyanyasaji wa kijinsia. Mathalani wanaweza kuwashauri wanawake wenzao kudumisha mila na desturi nzuri na kupiga vita mila potofu kama ya kukeketa wanawake, ndoa katika umri mdogo na ndoa za wake wengi.

## Mwanawake kama Mlezi

Baada ya kujifungua watoto wanawake wana wajibu wa kuwalea watoto ili waweze kukua katika maadili mema katika nyanja zote za maisha. Vilevile wanao wajibu wa kuwafundisha watoto wote namna ya kuishi kwa kuzingatia usawa wa kijinsia. Wajibu huu sio wa wanawake peke yao bali ni wa jamii nzima. Hata hivyo ni ukweli kuwa wanawake wanakaa na watoto kwa muda mwingi zaidi kuliko wanaume. Hivyo hawana budi kutumia nafasi hiyo kupambana na unyanyasaji wa kijinsia kuanzia ngazi ya familia hadi kitaifa.

## Mwanamke kama Mwanaharakati

Katika jamii nyingi mwanamke ndiye mtu wa kwanza na mwenye jukumu kubwa la kupambana na unyanyasaji wa kijinsia. Kwa mfano, mwanamke anapaswa kuwa wa kwanza kutoa taarifa za unyanyasaji wowote anaoshuhudia katika jamii yake.

# Sura ya Tatu

## Athari za ukiukwaji wa Usawa wa Kijinsia

### Maana ya Usawa wa Kijinsia

Usawa wa kijinsia ni hali ya ulinganifu kati ya mwanamke na mwanaume katika kutoa maamuzi mbalimbali katika jamii, kama vile mgawanyo wa mali. Usawa wa kijinsia unalenga kuleta ulinganifu na maelewano katika jamii baina ya mwanamke na mwanaume.

Kimantiki usawa wa jinsia ni hali ya maisha isiyojengeka katika kubagua mwanamke au mwanaume kutokana na jinsi yake. Kimaumbile binadamu huzaliwa na jinsi ya kike au kiume, lakini jamii hutafsiri ni nini maana ya kuwa mwanamke au mwanaume kwa kutoa haki tofauti, stahili tofauti, wajibu na hata thamani ya utu. Katika jamii nyingi tofauti hizi huashiria kujenga tabaka kati ya mwanaume na mwanamke kwa njia ya kuhalalisha ubaguzi wa jinsia ambao huashiria kumnyima mwanamke haki ya kufikia na kumiliki rasilimali na kupata heshima ya utu wake. Mfumo huu unapokithiri katika jamii huwa unadhoofisha kujengeka na kuimarika kwa demokrasia, utawala bora na uwajibikaji.

### Athari za ukiukwaji wa usawa wa kijinsia

Wanawake wengi bado wameonekana kuendelea kubaguliwa hasa katika suala la Kumiliki mali, kushiriki katika kutoa maamuzi, kupata elimu, Urithi wa mali n.k.

*hivyo kuendelea kuwa maskini siku hadi siku.*

**Ushiriki katika kutoa Maamuzi**

Ukiukwaji wa usawa wa [illegible]

kutoa maamuzi baina [illegible]

Athari [illegible]

**Kumiliki Mali**

Ukiukwaji wa usawa wa kijinsia unaathari kubwa katika umilikaji wa mali kati ya wanaume na mwanamke. Wanawake wengi wanakosa nafasi ya kumiliki mali kutokana na kutopewa fursa ya kumiliki mali hizo. Jamii nyingi za kiafrika ikiwemo Tanzania, zimekuwa zikitumia mila mbalimbali kumnyima mwanamke haki ya kumiliki mali katika familia. Dhana hii inaendelea kuwaathiri wanawake wengi na hivyo kuendelea kuwa maskini siku hadi siku.

**Ushiriki katika kutoa Maamuzi**

Ukiukwaji wa usawa wa kijinsia una athari kubwa katika kushiriki kutoa maamuzi baina ya mwanaume na mwanamke katika jamii. Athari mojawapo ya ukiukwaji wa usawa wa kijinsia ni kuwanyima wanawake nafasi ya kushiriki katika kutoa maamuzi mbalimbali katika jamii. Hali hii inamfanya mwanamke kuendelea kuwa mtumwa wa maamuzi ya wanaume.

**Upatikanaji wa Elimu katika Jamii**

Ukiukwaji wa usawa wa kijinsia unaathari kubwa ya upatikanaji wa elimu baina ya mwanaume na mwanamke katika jamii. Mara nyingi wanawake wamekuwa hawapewi nafasi sawa na wanaume katika kupata elimu. Wanawake wengi wamebaki nyuma kielimu kutokana na mfumo dume unaochochea vitendo vya ukatili dhidi ya watoto wa kike, na wanawake kwa ujumla. Vitendo hivi huchangiwa na changamoto mbalimbali katika jamii kama vile; maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi, umaskini na mila na desturi zilizopitwa na wakati. Mfano, kutokana na umaskini wazazi wengi wamekuwa wakiwatumia watoto wao wa kike kama chanzo cha kujipatia mali kwa kuwaozesha wakiwa na umri mdogo au kutowachukulia hatua zozote wanaume wanaowapa mimba

watoto wao. Vitendo hivyo vinasababisha asilimia kubwa ya wanawake kukosa fursa ya kupata elimu rasmi, na hivyo kuendelea kuwa masikini.

Aidha, wazazi wengi wamekuwa wakiendeleza au kuunga mkono vitendo hivi bila kujua madhara yake. Baadhi ya madhara yanayotokana na mimba za utotoni ni kama vile kukosa haki za msingi kwenye elimu, kupata shida wakati wa kujifungua kwani viungo vinakuwa havijakomaa na pia kuolewa katika umri mdogo. Hivyo basi, kuimarisha upatikanaji wa elimu kwa wanawake kutawainua kiuchumi, kwa kuwa elimu hutoa ujuzi, maarifa na hali ya kujiamini .

**Urithi wa Mali**

Ukiukwaji wa usawa wa kijinsia una athari kubwa katika kurithi mali baina ya mwanaume na mwanamke. Jamii nyingi zimekuwa hazitoi nafasi sawa ya kurithi mali kati ya mwanamke na mwanaume. Hali hii imeendelea kuwafanya wanawake wengi kuendelea kuwa maskini wakilinganishwa na wanaume

# Sura ya Nne

## Mifumo, Mila na Desturi zinazochangia Unyanyasaji wa Kijinsia

### Mifumo

Taarifa kutokana na tafiti zilizofanywa na TEWW zinaonesha kuwa wanawake asilimia 63 walitaja mfumo dume kutumiwa kama chanzo cha kuendeleza na kuchochea vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia. Hata hivyo vitendo hivi vimeonekana kufanyika katika nyanja zote za maisha zikiwemo mila na desturi, malezi na makuzi, elimu, sera na sheria.

### Mfumo Dume

Mfumo dume ni mfumo unaodumishwa katika jamii za aina mbalimbali. Lengo lake ni kuhakikisha kundi au makundi fulani yanapata kipaumbele katika kunufaika na rasilimali zilizopo. Kwa sababu za kihistoria wanawake hutumia muda mwingi kwenye shughuli za uendelezaji jamii, mchango wa wanawake kwenye maendeleo na shughuli za uchumi umefichika, hauthaminiwi wala kuhesabika kwenye pato la taifa. Kwa hiyo, hata suala la kuona wanawake wananufaika na rasilimali linakuwa halipo.

### Mila na Desturi

Baadhi ya mila na desturi za makabila mbalimbali nchini Tanzania zinachangia kushamiri kwa matendo ya ukatili wa kijinsia. Katika sura hii mila na desturi kama vile kutakasa wajane, kurithi wajane, ndoa za utotoni, ukeketaji wanawake na kuoa wake wengi zinajadiliwa

### Kutakasa Wajane

Baadhi ya makabila mume anapofariki ni lazima mjane atakaswe.

Kutakaswa ni hali ya mjane kujamiiana kimwili na mwanaume aliyechaguliwa na kijiji au ukoo ili kumwondolea mkosi alionao mjane huyo. Baadhi ya jamii zina mtu maalumu anayehusika na kutakasa na wakati mwingine mtu yeyote huchaguliwa ili kumtakasa mjane. Mtakasaji hujamiiana kwanza na mjane halafu anaenda kujamiiana na mkewe kisha anarudi tena kujamiiana na mjane. Hapo ndipo tendo la kutakasa linakua limekamilika. Tendo hili hufanyika kwa usiku mmoja tu na baada ya hapo mume aliyefariki anaruhusiwa kuzikwa na mjane kuolewa tena. Huu ni ukatili wa kijinsia kwani mwanamke hana nafasi ya kukataa tendo la kutakaswa bali anatakiwa akubali na kuonesha ushirikiano kwa huyo mwanaume aliyechaguliwa kumtakasa.

Mila hii inahatarisha maisha ya wanawake iwapo mwanaume anayepewa jukumu la kutakasa atakuwa na virusi vya UKIMWI. Hata hivyo, baadhi ya wanawake wamekuwa wakiathirika kisaikolojia.

**Kurithi Wajane**

Baadhi ya makabila nchini mume akifariki, ndugu wa marehemu hurithi mke wa marehemu, vilevile mke akifariki mume hupewa mdogo wa mkewe au ndugu wa karibu wa marehemu ili aweze kulea watoto. Huu ni ukatili wa kijinsia kwani anayerithiwa anakua hajapewa uhuru wa kukubali au kukataa bali ni amri na lazima atii. Kwa upande mwingine inaonekana mila hii ina lengo zuri lakini kwa sababu haimpi nafasi mwanamke huyo kuamua, basi huu nao ni ukatili wa kijinsia.

**Kukeketa Wanawake**

Ukeketaji ni kitendo cha kikatili sana kwani kinawapa wanawake ulemavu wa kudumu, kinawaweka wanawake katika hatari ya kuambukizwa magonjwa kama vile UKIMWI. Kitendo hiki ni ukatili

wa kijinsia kwani kinafanywa kwa wasichana bila ridhaa yao bali ni kutokana na utaratibu uliowekwa na mababu zao.
Jamii nyingi zinazoendeleza utamaduni huu wa kukeketa zimekuwa na dhana potofu ya kumtambua, kumpenda na kumthamini mwanamke au msichana aliyekeketwa. Dhana hii potofu imeendelea kuwa kichocheo cha ukeketaji wa wanawake katika jamii.

Baadhi ya mbinu zinazotajwa kutumiwa na "Mangariba"kama wanavyojulikana ni kama zifuatazo:

1. kuwazawadia baada ya kutahiriwa,
2. kuwaficha porini,
3. kuwatahiri kwa mtindo wa kisasa (hukata kidogo kwa juu),
4. kuwakeketa wakiwa bado wadogo, na
5. Kuwatishia kutengwa na ukoo au kutoolewa ikiwa hawatakeketwa.



*Kielelezo: Mila potofu za ukeketaji kwa watoto hazifai*

**Kuoa wake Wengi**

Kuna baadhi ya makabila mwanaume anayeoa wake wengi anaonekana ni mtu jasiri na anayeheshimika na jamii. Hivyo wanaume wengi wamejijengea utamaduni wa kuoa wake wengi ili kujijengea heshima katika jamii. Kwa upande mwingine baadhi ya wanawake wanaoolewa wanakuwa katika ukatili wa kijinsia kwani wengine wanashindwa kutoshelezwa kiunyumba na waume zao. Pia baadhi ya wanawake hawa hawaolewi kwa ridhaa yao ila ni kutokana na shinikizo la wazazi na jamii.

Mwenendo huu husababisha ndoa nyingi kuwa na migogoro ya mara kwa mara inayosababisha baadhi ya wanawake kuadhibiwa na waume zao

**Ndoa za Utotoni**

Baadhi ya makabila watoto huolewa wakiwa na umri mdogo ili wazazi waweze kupata fedha au mifugo kutoka kwa waoaji. Watoto wengi wameolewa na watu wazima wenye umri mkubwa, na hivyo kusababisha mimba za utotoni na kusababisha wengi wao kupoteza maisha. Huu ni ukatili wa kijinsia kwani wasichana wanaozeshwa bila ridhaa yao kwa watu wasiokuwa na mapenzi nao.



Kielelezo: *Msichana mdogo akinyonyesha mtoto*

# Sura ya Tano

## Jitihada Zinazofanywa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima katika Kuleta Usawa wa Kijinsia

Katika kutekeleza majukumu yake Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) kwa muda mrefu imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha inachangia kuleta usawa wa kijinsia kwenye jamii. Ikizingatiwa kwamba elimu ni chombo cha ukombozi, TEWW kupitia programu zake za elimu imekuwa ikibuni na kutekeleza miradi yenye lengo la kumkomboa mwanamke katika nyanja mbalimbali za maisha. Kuanzia mwaka 2013 hadi 2016 kwa mfano, miradi mitatu ya kielimu imeanzishwa na kutekelezwa katika mikoa mbalimbali ya Tanzania bara. Miradi hiyo ni pamoja na Elimu ya Sekondari kwa wasichana walio nje ya shule (Secondary Education for Out of School Adolescent Girls – SEOSAG), Elimu mbadala kwa wasichana waliokatisha masomo kwa sababu za ujauzito (2013-2015)-(Alternative Learning for Out of School Teenage Mothers-) na mwingine ni kuzuia ndoa za utotoni na za kulazimishwa ujulikanao kama "Wezesha Wasichana" – Girls Inspire.

### Elimu ya Sekondari kwa Wasichana Walio nje ya Shule

Mradi huu unatekelezwa na TEWW kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la BRAC Maendeleo Tanzania (BMT). Walengwa wa mradi huu ni wasichana walioshindwa kuendelea na elimu ya sekondari kutokana na sababu mbalimbali na hivyo kukosa fursa ya kupata elimu hiyo. Mradi huu unatekelezwa katika mikoa ya Singida, Shinyanga, Mwanza, Dar es Salaam, Tabora na Tanga. Lengo ni kuwafikia wasichana wengi kwa kutumia njia ya ujifunzaji huria na masafa. Katika mfumo huu wa ujifunzaji, wanafunzi hujisomea wenyewe katika vituo 150 vilivyoanzishwa kwenye maeneo yao

wakiongozwa na wawezeshaji jamii waliopewa mafunzo na wataalamu kutoka TEWW. Pia hukutana katika vipindi vya ana kwa ana mara mbili kwa mwezi.

**Elimu Mbadala kwa Wasichana Waliokatisha Masomo kwa sababu ya Ujauzito**

Mradi huu ulilenga kutoa fursa ya elimu kwa wasichana walioacha shule kwa sababu ya kupata ujauzito wakiwa shule ya sekondari. Ulilenga kuwafikia wasichana 200 katika Halmashauri za Shinyanga vijijini, Kahama mji na Msalala. Ni mradi uliofadhiliwa na shirika la UNESCO kwa kushirikiana na shirika la msaada la Japan (Japaness Trust Fund). Kwa kupitia mradi huu wasichana hawa walijifunza stadi za maisha na ufundi ili waweze kujitambua na kujiwezesha kiuchumi na hivyo kutoa mchango katika maendeleo ya jamii. Wasichana hawa waliwezeshwa kupata zana na vifaa vya ufundi ambavyo vilimilikishwa kwa vikundi 10 vilivyoanzishwa na kusajiliwa kama vikundi vya ujasiriamali kwenye maeneo yao. Kutokana na mradi huu wasichana wengi walijitambua na kuanzisha biashara zilizowawezesha kupata pesa za kulipia ada ya shule na hivyo kuendelea na masomo yao waliyokatisha kupitia mfumo wa elimu huria.

**Wezesha Wasichana (Girls Inspire)**

Huu ni mradi unaolenga kutoa elimu kwa wasichana na wanawake wapatao 3,000 wenye umri kati ya miaka 10 – 25 walio nje ya mfumo rasmi wa Elimu. Malengo ya mradi huu ni kuzuia ndoa za utotoni na za kulazimishwa katika mikoa ya Rukwa, Lindi na Dodoma. Mradi huu unatekelezwa na TEWW kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la KIWOHEDE na SIDO kwa ufadhili wa shirika la Elimu la Jumuiya ya Madola (Commonwealth of Learning – CoL).

Wasichana katika mradi huu watawezeshwa kupata elimu ya ujasiriamali, stadi za maisha, ufundi na pia kujiunga na masomo ya sekondari kwa njia ya huria na masafa kulingana na mahitaji yao ya kupata elimu.

Mfumo wa uendeshaji wa mafunzo haya unatumia teknolojia rafiki ambayo itawawezesha walengwa kujifunza kwa muda wao kwa kutumia masomo yaliyoandaliwa katika vipindi vya video na redio. Katika kutekeleza mradi huu, TEWW itahusika na usajiri wa walengwa, kujenga uwezo wa wawezeshaji na waendeshaji katika ngazi zote za uendeshaji na pia kuendesha mafunzo ya masomo ya sekondari huria. Ufundishaji wa stadi za ufundi wa awali utafanywa na SIDO wakati KIWOHEDE watashughulika na uhamasishaji wa jamii juu ya athari za ndoa za kulazimisha na mimba za utotoni.

# Sura ya Sita

## Jitihada za serikali na mashirika binafsi kupambana na unyanyasaji wa kijinsia

Katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo na usawa wa kijinsia hapa nchini Serikali imekuwa ikichukua hatua za utekelezaji katika maeneo mbalimbali, kama vile sheria ya makosa ya kujamiiana (SOSPA) ya mwaka 1998. Mkakati wa maendeleo ya Jinsia chini ya wizara ya maendeleo ya jamii, jinsia na watoto. Pia serikali kuunga mkono jitihada zinazofanywa na mashirika yasiyo ya kiserikali na wadau wengine.

### Kuwapa wanawake uwezo wa kisheria

Katika kuhakikisha kuwa wanawake wanajengewa uwezo wa kisheria na kupata haki zao. Sheria kadhaa zimetungwa na nyingine kufanyiwa marekebisho ikiwemo Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA) ya mwaka 1998, ambayo imefanyiwa marekebisho na kuhuishwa kwenye Sheria ya Kanuni za Adhabu; Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini Na. 6 ya mwaka 2004 ambayo imetoa fursa sawa katika ajira na likizo ya uzazi pamoja na Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009.

### Kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi

Katika kuhakikisha kunakuwa na ongezeko la ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi. Marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 yalifanywa mwaka 1995 na kuongeza viti maalum kwa wanawake vilivyoongezwa kuwa asilimia 15 ya viti vyote na kwa Zanzibar idadi ya nafasi za uwakilishi wa wanawake iliongezeka hadi asilimia 20 mwaka 2000. Mabadiliko mengine ya Katiba ya

mwaka 1977 yalifanywa mwaka 2005 na kuongeza viti maalum 15 vya wabunge kufikia asilimia 30. Aidha, kwa mujibu wa katiba hiyo, Mheshimiwa Rais amepewa mamlaka kuteua wabunge 10. Kati ya hao, wabunge watano ni lazima wawe wanawake. Kufuatia marekebisho hayo idadi ya wabunge wanawake kwa sasa ni asilimia 36.

**Kuwawezesha wanawake kiuchumi**

Katika kuwawezesha wanawake kiuchumi Serikali imeanzisha Mfuko wa Maendeleo ya wanawake unaotoa mikopo ya kuanzisha biashara na shughuli nyingine za kiuchumi. Vilevile, Serikali imeandaa Sera ya Mitaji midogomidogo ya mwaka 2000, ambayo imeweka mazingira mazuri kwa taasisi binafsi za kifedha ambazo nazo hutoa mikopo kwa wanawake. Kwa mfano, Bank ya Wanawake Tanzania (TWB) kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba, 2013 ilitoa mikopo kwa wanawake 7,395 yenye thamani ya shilingi bilioni 9.163 na pia walipatiwa mafunzo ya ujasiliamali. Wanawake hao ni sawa na asilimia 79 ya wateja wote waliopewa mikopo. Taasisi nyingine zinazotoa mikopo kwa wanawake ni pamoja na PRIDE, FINCA, GATSBY- TANZANIA, SELF na kadhalika.

**Kuwapa wanawake nafasi katika elimu na mafunzo**

Elimu ya Msingi: Haki ya kupata elimu ni haki ya kibinadamu na yenye maana kubwa kwa mtu binafsi pamoja na maendeleo ya kiuchumi. Katika elimu yapo mafanikio makubwa. Takwimu zinaonesha kuwapo na uwiano sawa (kwa tofauti ya 0.99) kwa wasichana na wavulana wanaojiunga na elimu ya msingi, *kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi kwa mwaka 2012.*

Stadi za ufundi; wasichana wamekuwa mstari wa mbele katika kujiunga na stadi za ufundi, kwa mfano wasichana wenye umri kati ya miaka 7-13. Aidha wasichana wamekuwa wakiongezeka katika mafunzo ya ufundi kutoka asilimia 88.7 (mwaka 2006) hadi kufikia asilimia 89.6 (mwaka 2010).

Elimu ya Sekondari: idadi ya wanafunzi wanaojiunga na shule hizi iliongezeka kutoka wanafunzi 675,672 mwaka 2006 hadi wanafunzi 1,638,699 mwaka 2010. Kwa mwaka 2006 wavulana walikuwa 358,128 sawa na asilimia 53 na wasichana walikuwa 317,544 sawa na asilimia 47. Mwaka 2010 kulikuwa na ongezeko ambapo wavulana walikuwa 910,171 sawa na asilimia 56 na wasichana walikuwa 728,528 sawa na asilimia 44. Kwa kiwango kikubwa uamuzi wa Serikali wa kuanziasha shule za sekondari za kata na uhamasishaji vilisaidia kuongeza idadi ya wasichana na wavulana waliojiunga na elimu ya sekondari.


Masomo ya Chuo Kikuu: Udahili wa wanafunzi katika vyuo vikuu vya Serikali na Binafsi. Jumla ya wanafunzi 118,951 walidahiliwa mwaka 2009/2010. Kati yao wavulana walikuwa 76,935 sawa na asilimia 67.8 na wasichana 42,016 sawa na asilimia 32.2. Aidha, vyuo vikuu vya binafsi vilidahili wasichana asilimia 40.5 na vile vya Serikali vilidahili wasichana asilimia 33.4. Uanzishwaji wa shule za sekondari za kata umewezesha wasichana wengi kupata elimu ya sekondari, hivyo kupunguza tatizo la kuolewa na kupata ujauzito katika umri mdogo.

Ajira; Sera ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Ajira ya mwaka 2002 inabainisha haki sawa za ajira kwa wanawake na wanaume. Aidha, sheria ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2002,

(iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2007) imetoa fursa sawa za ajira kati ya wanawake na wanaume. Inapotokea kuwa mwanaume na mwanamke wanapata alama sawa wakati wa usaili, mwanamke anapewa kipaumbele kupata nafasi hiyo. Pia, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (2004) imetoa fursa sawa kati ya wanawake na wanaume kuhusu haki zao za ajira, ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa likizo ya uzazi kwa wanawake na wanaume.

**Kupiga vita ukatili wa kijinsia**

Katika kukabiliana na kuonekana kwa tatizo la muda mrefu la unyanyasaji dhidi ya wanawake kutokana na mila na desturi potofu hapa nchini, Serikali imeandaa, sera, sheria na mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na Sera ya Maendeleo ya Jinsia na Wanawake (2000), Mkakati wa Kukabiliana na Ukatili wa Kijinsia (2001 – 2015) na Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA1998). Pia kwa kushirikiana na wadau kampeni mbalimbali za kupiga vita ukatili wa kijinsia zimeendeshwa kwa lengo la kuhamasisha jamii kuacha ukatili dhidi ya wanawake na wasichana na uhamasishaji huu unafanyika kwa ushirikiano wa karibu sana na vyombo vya habari.



*Kielelezo: Adhabu kama hizi huashiria unyanyasaji kwa watoto*

Mafunzo yanayohusu kuzuia ukatili dhidi ya wanawake yanaendelea kutolewa kwa wasimamizi wa sheria, wakiwamo askari polisi, mahakimu wa wilaya, viongozi wa vijiji na Kamati za ulinzi na usalama. Jeshi la Polisi limeanzisha madawati ya Jinsia zaidi ya 417 na yanatoa huduma kwa wanaofanyiwa ukatili wa kijinsia.

Aidha Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa asasi zisizokuwa za serikali kushiriki katika kupiga vita ukatili wa kijinsia. Taasisi hizo zimekuwa na mchango mkubwa katika kutoa elimu, ushauri wa kisheria na matunzo kwa waathirika wa ukatili.

Kuanzishwa kwa madawati ya jinsia katika Wizara na Idara za Serikali, Wakala, Sekretariati za Mikoa na Halmashauri kunasaidia sana katika kuingiza masuala ya jinsia katika sekta husika. Aidha, baadhi ya Wizara na Taasisi nyingine zimeunda kamati za jinsia ndani ya Sekta zao ili kuharakisha uingizwaji wa masuala ya jinsia katika mipango ya kisekta, pamoja na upatikanaji wa takwimu zilizoainishwa kijinsia.

TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA
S.L.P 20679
Dar es Salaam, Tanzania